

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. HWT/L17/87

05.05.2023

KUSITISHWA KWA TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime alitangaza nafasi za kazi za Watendaji wa Vijiji 12 kupitia tangazo lenye Kumb. Na. HWT/L17/86 la tarehe 18.04.2023 baada ya kupokea kibali cha ajira mpya kwa mwaka 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime amepokea maelekezo kutoka kwa Katibu wa Sekretarieti ya ajira katika Utumishi wa Umma kuwa, kwa mujibu wa Kanuni Na. 22(1-2) ya Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Sekretarieti ya ajira kama ilivyorekebishwa kupitia gazeti la Serikali Na.580 la 2022 kuwa inaelekeza kutumika kwa kanzi data ya waliofaulu usaili na hawakupangiwa vituo vya kazi pale inapotokea fursa ya ajira.

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ilitangaza nafasi 14 mwaka wa 2021/2022 na kufanya usaili ambapo wasailiwa wengi walifaulu na kwa kuwa nafasi zilikuwa chache hawakupangiwa vituo vya kazi.Hivyo, wasailiwa hao waliofaulu na kukosa fursa ya kuajiriwa wataitwa kujaza nafasi12 zilizotangazwa. Kwa maelezo haya ninasitisha maombi ya nafasi za ajira ya Watendaji wa Vijiji zilizotangazwa kupitia tangazo Kumb. Na. HWT/L17/86 la tarehe 18.04.2023.

Naomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

Solomon I. Shati
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
TARIME